**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 1**

# 1 Uumbaji



## Marejeo

Mwanzo 1 na 2:1 - 7

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu aliumba kila kitu nchini, baharini na mbinguni.

## Maneno maalum

1 Mungu + Muumba + Biblia + asili (chanzo)
2 Giza + mwangaza (nuru) + uwezo (nguvu za) wa Mungu - siku ya 1
3 Hewa + anga + mbingu - siku ya 2
4 Bahari + ardhi (nchi) + mimea + miti - siku ya 3
5 Jua + mwezi + nyota - siku ya 4
6 Wanyama + ndege + samaki - siku ya 5
7 Mtu (mwanamme) + udongo (mchanga) + pumzi ya Mungu + Adamu
8 Mwanamke + ubavu wa Adamu + Hawa - siku ya 6
9 Mumgu alistarehe +siku maalum + tupeane shukrani - siku ya 7

## Maswali

1 Ni nani aliumba dunia na ni wapi tunaambiwa hayo?
2 Mwanzo ina maana gani?
3 Ni nini iliumbwa siku ya kwanza, siku ya pili na siku ya tatu?
4 Nini iliumbwa siku ya nne na siku ya tano?
5 Ni kiumbe kipi kilicho maalum kilichuombwa siku ya sita?
6 Jina la hiki kiumbe ni nani?
7 Mungu alitengenezaje Adamu?
8 Mungu alitengenezaje Hawa?
9 Mungu alifanya nini siku ya saba?
10 Nasi tufanye nini kwa hiyo siku?

## Majibu

1 Biblia inatuambia kwamba Mungu aliumba dunia. Tunaambiwa kwa kitabu cha Mwanzo
2 Mwanzo inamaanisha kuanza
3 Aliumba siku ya kwanza nuru, siku ya pili hewa, anga na mbigu. Siku ya tatu miti, mimea, nyasi na mbegu.
4 Siku ya nne jua, mwezi na nyota. Siku ya tano wanyama, ndege na samaki
5 Mungu alifanya mtu siku ya sita
6 Kiumbe hiki alikiita Adamu
7 Mungu alitengeneza Adamu kutoka kwa udongo na pumzi ya uhai kutoka kwake tena
8 Mungu alitengeneza Hawa kutoka kwa ubavu wa Adamu
9 Mungu alistarehe siku ya saba
10 Tunatakiwa kuomba na kushukuru Mungu

Kila siku twona ndege, miti, maua, viumbe vidogo vidogo. Wakati mwingine twaona samaki. Tunaona rangi za kupendeza. Tunaona vingine ni vikumwa na vingine ni vidogo. Tunawaza - jinzi gani hivi vitu vizuri vilianza au vilipatikana.

**1.1** Tukitaka ukweli, tusome Biblia. Biblia inatueleza ni nini Mungu anatufanyia. Inatueleza ni nini nasi tunaweza kumfanyia Mungu. Ina twambia kwamba, Mungu ni muumba. Mwanzo ni kitabu cha kwanza katika Biblia. Maana yake ni chanzo au asili au kuanza.

**1.2** Hapo mwanzo dunia ilikua giza na maji yalizunguka zunguka kila pahali. Mungu akasema, "Nuru ije." Nuru ikaja kwa uwezo (nguvu) wa Mungu. Kukawa na wakati wa giza na wakati wa nuru. Mungu akaita giza, usiku na nuru mchana. Hiyo ilikuwa siku ya kwanza.

**1.3** Siku ya kufuata Mungu akagawanyisha hayo maji ili kuwe na nafasi kubwa ya hewa na anga. Hii akaiita mbingu. Hiyo ilikuwa siku ya pili.

**1.4** Siku ifuatayo Mungu kwa uwezo wake akakusanya maji yale yazungukayo pamoja. Akaiona ardhi. Akaita yale maji bahari na ile ardhi akaita nchi. Kwa nchi akafanya nyasi na mbegu. Akafanya kila aina ya mimea na mbegu yake. Akafanya miti yote na matunda yake. Miti ya machungwa, mkomba ya ndizi, miti ya maembe n.k (etc) Mungu akaangalia kila kitu na vyote vilionekana vizuri. Hiyo ilikuwa siku ya tatu.

**1.5** Tena huko katika mbingu, Mungu akaweka vyombo viwili vya mwangaza kuu. Angalau moja ilikua na mwangaza mwingi kuliko ingine. Ya mwangaza zaidi ni jua ingine ni mwezi. Akaweka pia nyota. Hii ilikuwa siku ya nne.

**1.6** Sasa nchi ilikuwa tayari kuwa na viumbe vyote, kulikua na hewa ya kupumua, vyakula vingi vya kukula, mbega yote, matunda yote, nyasi yote, kwekwe za bahari na jua linawaka. Hebu fikiria ndege na samaki wa aina yoyote wenye umeshaona. (uliza watoto wapeane majibu). Kuna wengi wenye hatujawahi kuwaona. Mungu alifanya wote. Mungu alifanya viumbe vya kiume na vya kike. Mungu alivizungumuzia na kuvibariki, na ni lazima viwe na jamii. Samaki wajaze bahari na ndege watawanyike katika nchi. Hiyo ilikuwa siku ya tano.

**1.7** Mungu kwa nguvu zake alikuwa tayari kufanya kila aina ya mnyama (fikiria wanyama wowote unaowajua). Wanyama walikuwa na vyakula vyao. Mungu ni wa ajuba kweli. Alikua tayari kutengeneza viumbe maalum wawili. Mtu mwanamme na mwanamke. Mwanzo 2:7 Inatueleza vile mtu wa kwanza aliumbwa. Mungu alitengeneza umbo la mtu kutoka kwa udongo wa chini. Baadaye Mungu akampulizia pumzi yake ndani ya pua mpaka kwa mapafu. Mtu akawa hai. Mungu akafaya viumbe vyote kwa njia hii. Soma Mwanzo 2:19).

**1.8** Mungu akampa huyo mtu mwanamme jina. Aliitwa Adamu. Adamu alihitajika awe na rafiki. Mungu akamtengenezea mwanamke wa kwanza. Alitengenezwa kwa njia maalum. Mungu alimfanya Adamu akalala. Akachukua ubavu kutoka kwake na kufanya mwanamke. Akampulizia pumzi yake. Hapo kukawa na mwanamke aliyeitwa Hawa. Soma Mwanzo 3:20.

Mungu aliagalia kila kitu alichofanya na vyote vilikuwa vizuri sana. Hiyo ilikuwa siku ya sita. Mungu aliwaambia Adamu na Hawa wawe na jamii. Walihitajika kujaza watu katika nchi.

**1.9** Baadaye kukaja siku ya saba. Siku hii Mungu alistarehe. Akaifanya hii siku kuwa maalum. Siku iliyokuwa tofauti na siku zingine.

Mungu alifikiria juu ya vitu vyote alivyovifanya. Nasi tunaweza kuwa na siku maalum, tufikirie juu ya nini Mungu ametufanyia. Tushukuru kwa hii siku na siku zingine zote.

Hapa tunafaa (tunastahili) kuomba Mungu na tumshukuru kwa kuumba kila kitu.